



*Taarifa kwa umma, Alhamisi, 23 Decemba 2010*

## **Uhaba wa Wafanyakazi wa Afya, ni Kushindwa kwa Serikali Kuwajibika**

Maafisa utumishi wa halmashauri na watumishi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wanapaswa kuangalia mafanikio yao kwa kutatua tatizo la uhaba wa wafanyakazi wa afya, ambalo linarudisha nyuma ubora na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya. Wanapaswa kushirikiana kwa ukaribu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MOHSW) pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuajiri wafanyakazi wapya kwa kuzingatia mahitaji na maombi ya Halmashauri ya kila mwaka.

Kufuatia ziara ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ya hivi karibuni katika Hospitali ya Temeke, utoaji wa huduma za afya chini ya viwango na tatizo sugu la uhaba wa wafanyakazi katika hospitali hiyo viligundulika. Wakati watumishi wa Wizara ya Afya wakielekeza lawama kwa Mkurugenzi wa Manispaa kwa kutoomba wafanyakazi wa afya wa kutosha, vyombo vya habari vilimnukuu Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Steven Kongwa akisema kwamba katika mwaka wa fedha 2009/10, waliomba wafanyakazi wa afya 250 na kupewa wafanyakazi 20 tu.

Kufuatia mkanganyiko wa taarifa hizo, Sikika, asasi isiyo ya kiserikali inayochochea utawala bora katika sekta ya afya, ilifanya uchambuzi wa mipango ya rasilimali watu kwa kuangalia mipango ya afya ya kila mwaka katika halmashauri 32 za Tanzania. Hii ilifuatiwa na mahojiano na baadhi ya viongozi kutoka ngazi mbalimbali za serikali. Matokeo ya uchambuzi huu yamebainisha matatizo ya aina mbalimbali yanaegemea katika ngazi mbalimbali za serikali.

Kwanza, idara za afya haziandai mipango ya afya ya kila mwaka yenye uhalisia na ubora unaotakiwa hivyo serikali kuu hupotoshwa kuhusu aina na ukubwa wa matatizo mbalimbali ya afya katika ngazi ya halmashauri. Mipango mingi hunakiliwa kutoka mipango ya miaka iliyopita na kurudiwa katika miaka inayofuata. Taarifa na takwimu za kila mwaka hazibadilishwi na mara nyingi huwa na makosa ya kimahesabu. Kwa Manispaa ya Temeke, hakuna ushahidi wa maombi rasmi ya wafanyakazi wa afya 250. Idadi hii ilitajwa katika mpango wa afya wa Wilaya wa mwaka 2009/2010, ambayo sio mara zote huwasilishwa kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Pili, hata kama hesabu zilikuwa sahihi, maafisa utumishi wa halmashauri mara nyingi hawawasilishi maombi yao halisi ya rasilimali watu kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama inavyopangwa kila mwaka. Kwani mamlaka ya kutoa kibali cha ajira yapo kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tatu, hata kama maombi halisi ya kila mwaka yamewasilishwa kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kibali cha kuajiri kitatolewa tu na Menejimenti hiyo, kufuatia vigezo visivyo kuwa wazi.

TAMISEMI na Wizara ya Afya zinaweza kusaidia Halmashauri kukubaliana juu vibali vya kutosha vya ajira na Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Tunaamini, wizara zote zina Idara ya Utawala na Utumishi zenye wafanyakazi wenye uwezo na wenye kuitambua sera ya ajira ya serikali na taratibu zake. Ni jukumu la pamoja kati ya TAMISEMI na Wizara ya afya kuhakikisha utoaji wa huduma bora ya afya katika ngazi ya halmashauri.

Sikika inawakuwakumbusha viongozi wote wanaohusika kuwa wafanyakazi wa afya ni muhimu katika mfumo wa utoaji wa huduma za afya na upungufu wao unapunguza ubora na wingi wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi. Menejimenti ya Utumishi wa Umma inawajibika mkubwa katika hili wakati TAMISEMI na Wizara ya Afya wanapaswa kutoa ushirikiano mzuri. Ubora na mipango sahihi katika ngazi ya wilaya ni muhimu, pia maafisa utumishi katika kila halmashauri wanapaswa kutekeleza majukumu yao.

Kushindwa kuajiri wafanyakazi wa afya wa kutosha na wenye sifa katika ngazi zote za utoaji wa huduma ya afya ni kushindwa katika utoaji wa huduma hivyo kupelekea Serikali kushindwa kuwajibika kwa wananchi wake.

Mr Irenei Kiria

Mkurugenzi Mtendaji Sikika, P.O.Box 12183 Dar es Salaam,

Simu: +255 222 666355/57, Fax: 2668015, barua pepe: info@sikika.or.tz, Tovuti: [www.sikika.or.tz](http://www.sikika.or.tz)